

HOTUBA YA IJUMAA.

Kanuni za ujenzi wa familia na njia za kuilinda.

Imefasiriwa

Na

Profesa Ayman Alasar

Shukrani zote ni za Mwenyezi Mungu Mola wa viumbe wote. Mwenye kusema ndani ya Kitabu chake Kitakatifu:

وَمِنْ آيَاتِهِ أَنْ خَلَقَ لَكُمْ مِنْ أَنفُسِكُمْ أَزْوَاجًا لِتَسْكُنُوا إِلَيْهَا وَجَعَلَ بَيْتَكُمْ مَوَدَّةً وَرَحْمَةً إِنَّ فِي ذَلِكَ لَآيَاتٍ لِقَوْمٍ يَتَفَكَّرُونَ.

{Na katika alama zake ni kukuumbieni wake wanaotokana na nyinyi ili mpare utulivu kwao na akafanya kati yenu mapenzi na huruma, hakika katika hayo kuna alama kwa watu wenye kufikiri}. Ninashuhudia kuwa hakuna mola wa haki ispokuwa ni Mwenyezi Mungu peke yake hana mshirika, na ninashuhudia kuwa Mtume Muhammad ni Mtume wake na mja wake, ewe Mwenyezi Mungu peleka rehma amani na baraka kwake na kwa watu wa nyumbani kwake pamoja na kwa Maswahaba zake na wale wenye kuwafuata kwa wema mpaka siku ya kiyama.

Baada ya utangulizi:

Uwepo wa familia katika maisha ya mwanadamu ni miongoni mwa neema kubwa za Mwenyezi Mungu Mtukufu, kwani Mwenyezi Mungu ameitaja neema hii kwa waja wake ndani ya Kitabu chake Kitukufu, ambapo Anasema Mwenyezi Mungu Mtukufu:

وَاللَّهُ جَعَلَ لَكُمْ مِنْ أَنفُسِكُمْ أَزْوَاجًا وَجَعَلَ لَكُمْ مِنْ أَزْوَاجِكُمْ بَنِينَ وَحَفَدَةً وَرَزَقَكُمْ مِنَ الطَّيَّابَاتِ أَفَبِالْبَاطِلِ يُؤْمِنُونَ وَبِنِعْمَتِ اللَّهِ هُمْ يَكْفُرُونَ.

{Na Mwenyezi Mungu amekuumbieni wake katika jinsi yenu, na akakujaalieni kutoka kwa wake zenu watoto na wajukuu, na akakuruzukuni vitu vizuri vizuri. Basi je, wanaamini upotovu na wanazikataa neema za Mwenyezi Mungu}.

Familia ndio kiini cha jamii, na nguzo ya kwanza ya kulinda jamii, hivyo Uislamu umetoa umuhimu mkubwa wa kuijenga kwa ujenzi imara wenyewe kushikana na kufikia upendo na huruma kati ya watu wake, hivyo kupelekea kuenea kwa usalama na utulivu wa jamii nzima, ambapo Sharia ya Kiislamu imekuja na umuhimu wa kuteua mshirika wa maisha kwa uangalifu mkubwa unaopelekea utulivu wa maisha ya ndoa, kama vile imesisitiza juu ya umuhimu wa kufikia uwezo wa kubeba majukumu ya familia kwa pande zake zote za kifedha kijamii na kinafsi, ambapo anasema Mtume wetu Mhammad S.A.W: “*Enyi vijana mwenye kuweza mionganoni mwenu kuo basi na aoe, kwani kufanya hivyo kunapeleka kufunika macho na kulinda tupu, na asiyeweza kuo basi anapaswa awe anafunga kwani kufanya hivyo kwake ni kinga*”.

Sharia ya Kiislamu imesisitiza uangalifu wake kwenye malezi mema na mazuri ya watoto, na kuwajengea hisia za majukumu yao kwenye dini yao, jamii yao na taifa lao, jambo linaasisi ujenzi wa familia yenye nguvu na iliyosawa kupitia kusimika misingi ya kidini na kijamii, mila na desturi zenyeye manufaa kwenye nafsi za watoto, kwani wao ni amana kwenye shingo za wazazi wao, ambapo Anasema Mwenyezi Mungu Mtukufu: يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آتَمُوا قُوَّاً نَفْسَكُمْ وَأَهْلِكُمْ تَارًا وَقُوْدُهَا النَّاسُ وَالْحِجَارَةُ {Enyi mliaoamini ziokoeni nafsi zenu familia zenu na adhabu ya moto, kuni zake na watu na mawe}. Na anasema Mtume S.A.W “*Mwenyezi Mungu ni Mwenye kumuuliza kila mchuga kuhusu kile alichokichunga, alikilinda au alikipoteza? Mpaka atakuja kumuuliza mtu kuhusu watu wa nyumbani kwake*”. Kama vile watoto wema wanakuwa ni tulizo la macho ya wazazi duniani na Akhera, ambapo Anasema Mwenyezi Mungu Mtukufu:

وَالَّذِينَ يَقُولُونَ رَبَّنَا هَبْ لَنَا مِنْ أَرْوَاحِنَا وَدُرِّيَاتِنَا قُرْةً أَعْيُنٍ وَاجْعَلْنَا لِلْمُتَقِينَ إِمَامًا.

{Na wale wanaosema ewe Mola tupe sisi kutoka kwa wake zetu na vizazi vyetu kitulizo cha macho na utufanyie viongozi wacha-Mungu}. Na anasema Mtume S.A.W: “*Pindi anapofariki mwanadamu matendo yake yote yanakatika isipokuwa mambo matatu ndio yanabakia: Sadaka yenye kuendelea, au elimu itakayonufaisha, au kuacha mtoto mwema atakayemuombea dua*”.

Na Mtume S.A.W ametubainishia kuwa mtu bora mwanamme au mwanamke ni yule aliyebara kwa familia, ambapo anasema Mtume S.A.W خَيْرُكُمْ حَيْرُكُمْ لَأَهْلِهِ “*Mbora wenu ni yule mbora wenu kwa familia yake*” na Mtume S.A.W aliquwa ni

mtu bora kwa familia yake kwani alikuwa ni mume bora baba bora na babu bora, kwani asiyekuwa na kheir kwa familia yake basi huyo hana kheir kabisa.

HOTUBA YA PILI:

Shukrani zote anastahiki Mwenyezi Mungu Mola wa viumbe vyote, rehma na amani zimwendee mbora wa viumbe naye ni Mtume Muhammad pamoja na watu wa nyumbani kwake na Maswahaba zake wote.

Hakika Uislamu umetoa uzito mkubwa kwenye kulinda familia, yenyе kushikana na kusimama kwenye upendo na kuheshimiana, mwenye kuzingatia ndani ya Quran Tukufu atakuta kuwa imemwita mwanamke mshirika kwa mwanaume, wala hakuna neno hata moja linalomwita mke, kana kwamba Quran Tukufu imechukuwa usawa wa kilugha na kimaneno kama ishara na dalili ya uwiano wa kimaana, ambapo Anasema Mwenyezi Mungu: **{هُنَّ لِيَسُ لَكُمْ وَأَنْتُمْ لِيَسُ لَهُنَّ Wao ni vazi kwenu na nyinyi ni vazi kwao}**. Na Anasema tena: **{وَاهُنَّ مِثْلُ الَّذِي عَلَيْهِنَّ بِالْمَعْرُوفِ Nao wanawake wanayo haki kwa Sharia kama ile haki iliyo juu yao}**. Na Anasema Mwenyezi Mungu: **{لِلرِّجَالِ نَصِيبٌ مِّمَّا اكْتَسَبُوا وَلِلِّسَاءِ نَصِيبٌ مِّمَّا اكْتَسَبَنَ** {Wanaume wana fungu katika walio vichuma, na wanawake wana fungu katika walio vichuma}. Na anasema Mtume S.A.W katika hotuba yake kwenye hija ya kuaga: “**أَلَا إِنَّ لَكُمْ عَلَى نِسَاءِكُمْ حَقًا، وَلِنِسَاءِكُمْ عَلَيْكُمْ حَقًا**” **Fahamuni kuwa nyinyi kwa wake zenu muna haki, na wake zenu kwenu wana haki**”.

Mambo kati ya mume na mke yanasmama kwenye msingi wa utulivu upendo na huruma pamoja na kuchunga haki na wajibu, mbali kabisa na aina zote za kujitkuza, na maisha ya kifamilia hayawezi kuwa na utulivu katika mazingira ya kukweza kujitkuza na kutenza nguvu, bali huwa na utulivu katika mazingira ya kuheshimiana na kufanya kazi kwa pande zake zote ya kutengeneza bashasha na

kubeba mazito pamoja na kupambana na changamoto, na Abu Dardai alikuwa anasema kumwambia mkewe: Pindi ukiniona nimekasirika basi nisamehe, na pindi nikikuona umekasirika nikusamehe kinyume na hivyo hatutachukuliana.

Uzuri ulijoje familia kuishi kwenye utulivu furaha na amani, ili kufikia furaha duniani na Akhera.

**Ewe Mola wetu tupatie kwa wake zetu na watoto wetu utulivu wa macho na
utujaalie viongozi wacha-Mungu.**